

'Unapoteza wakati wako bure! Hakuna atakayekuamini': Usawiri wa Ubakaji katika Riwaya Teule za Kiswahili

Ernesta S. Mosha

Ikisiri

Makala haya yanajadili tatizo la ubakaji kama liliwyosawiriwa katika riwaya teule za Kiswahili. Kwa kutumia kilongo cha ashiki ya kujamiihana, makala yanaweka wazi mbinu mbalimbali zinazotumiwa na waandishi na kuwafanya wabakaji kuonekana kuwa hawana makosa huku wanawake wanaobakwa wakibebeshwa lawama kutokana na unyanayasaji wanaopata. Mwandishi wa makala anaeleza kuwa usawiri wa aina hii unaendeleza unyanyasaji wa wanawake na unarudisha nyuma juhudzi za jamii katika kuleta usawa wa wanawake na wanaume. Athari kubwa inayoweza kutokana na usawiri huu ni kuhalalisha unyanyasaji wa wanawake katika jamii inayolea na kuendeleza vitendo hivi vya kinyanyasaji. Aidha, makala yanabainisha kuwa riwaya zinaweza kutumika katika harakati za kupambana na tatizo hili la ubakaji kwa kusawiri mbinu zitakazowasaidia wanajamii kukomesha ubakaji pamoja na kukosoa vilongo vinavyoendeleza ubakaji kwa kuchomoza na kushadidia vilongo mbadala vinavyowaelimisha wanajamii namna wanavyoweza kuunga mkono harakati za kutokomeza aina hii ya unyanyasaji katika jamii ya Tanzania.

1.0 Utangulizi

Katika malengo ya milenia, lengo kuu la tatu ni kukuza usawa kati ya wanaume na wanawake na kuwawezesha wanawake kushiriki katika shughuli mbalimbali za kukuza uchumi katika jamii. Ni wazi kuwa lengo hili haliwezi kufikiwa kama bado tatizo la ubakaji linaendelea. Ubakaji unatambulika ulimwenguni – katika nchi zilizoendelea na zinazoendelea kama tatizo linaloathiri afya na linaloingilia haki za binadamu; na ni tatizo linalomwathiri mhanga kimwili, kiakili na kisaikolojia (Gavey, 2009; Jewkes na wenzake, 2006). Aghalabu, huwa na madhara ya muda mfupi na mrefu. Ingawa takwimu kuhusu upana wa tatizo la ubakaji zinakinzana kutokana na mbinu zinazotumika kupata taarifa pamoja na fasili ya maana ya ubakaji,¹ tafiti nyingi zilizofanyika kwa kutumia sampuli ya makazi, zinaonesha kuwa ubakaji katika maisha ya wanawake ni kati ya asilimia 10 na 21(Muganyizi, 2010). Muganyizi na wenzake (2004), wanaeleza kuwa

¹ Kwa kuwa kuna fasili nyingi kuhusu ubakaji, makala haya yanafasili ubakaji kama kitendo cha kumwingilia mwanamke kingono bila yeye mwenyewe kuridhia – kunahusisha matumizi ya nguvu, vitisho, ushawishi au wakati mwanamke hajitambui kutokana na ama kulewa au kuumwa.

asilimia 92 ya watuhumiwa wa ubakaji ni wanaume wanaojulikana na mhanga. Katika utafiti wao, Muganyizi na wenzake (2004) wanaeleza kuwa kati ya wanawake 142 walioeleza kuwa walibakwa, wanawake 129 sawa na asilimia 90.8 wana umri kati ya miaka 12 na 30. Hii inaonesha kuwa kundi kubwa la wanaobakwa ni wasichana walio katika umri mdogo. Tafiti zinaonesha kuwa kutokana na ukaribu kati ya mhanga na mbakaji na unyanyapaa uliopo katika jamii, wahanga wengi wa ubakaji hawatoi taarifa kwa kuhofia kutengwa na kupata aibu (Plummer na wenzake, 2007). Akieleza ugumu wa kupata takwimu halisi za tatizo la ubakaji nchini Tanzania, Muganyizi (2010) anabainsha kuwa taarifa zinazoripotiwa katika vituo vinavyoshughulikia ubakaji ni kati ya asilimia 2 - 20, wakati taarifa zinazotolewa kwa marafiki ni kati ya asilimia 59 - 91.

Wakizungumzia suala la unyanyasaji wa kingono shulen, Wubs na wenzake (2009), wanaeleza kuwa wanafunzi wa kiume wamekuwa wakiwanyanya wanafunzi wa kike na hivyo kufanya washindwe kusoma kwa amani. Katika utafiti wao uliohusisha nchi za Tanzania na Afrika ya Kusini, wanaonesha kuwa asilimia 61.3 ya wanafunzi wa kiume wa Tanzania (Dar es Salaam) waliohojiwa walieleza kuwa wamewanyanya wanafunzi wa kike kingono. Wanafafanua zaidi kuwa wanafunzi waliojihusisha zaidi na unyanyasaji wa kingono ni wale ambao wazazi wana uwezo kiuchumi. Matokeo haya yanafanana na yale ya Jewkes na wenzake (2006) kuwa wanafunzi wengi wanaojihusisha na ubakaji ni wale ambao wazazi wao wana kipato cha juu hususan kinachotokana na elimu. Aidha, ripoti ya Antonowicz (2010) inaeleza kuwa nchini Ghana, asilimia 14 ya matukio ya ubakaji yanafanywa na wanafunzi wa kiume. Kutokana na ukubwa wa tatizo la ubakaji katika jamii, kuna haja ya kutumia mbinu anuwai katika kutafuta ufumbuzi. Ni dhahiri kuwa kwa kuunganisha nguvu tunaweza kuelewa kwa mapana mbinu mbalimbali wanazotumia wabakaji lakini pia kuibua mbinu mbadala za kupambana na tatizo hili ambalo linakwamisha malengo ya milenia. Ni katika msingi huu, makala haya yanachangia katika harakati za kutafuta mbinu za kupambana na tatizo la ubakaji katika jamii ya Tanzania kwa kuchunguza namna waandishi wa riwaya za Kiswahili wanavyosawiri tatizo la ubakaji katika kazi zao ili kuona namna tunavyoweza kutumia kazi hizi za bunilizi katika kukabiliana na tatizo hili.

Kwa hiyo, makala haya yanamakinikia suala hili la ubakaji kwa kuchunguza namna riwaya² za Kiswahili zinavyoangazia suala hili la ubakaji. Kwa nini riwaya? Hayawaka (1990) anaeleza kuwa kazi za bunilizi hususan riwaya zinaathiri namna ya kufikiri, mtazamo na hata tabia. Anafafanua kuwa wale wanaosoma bunilizi nzuri siyo tu wanaweza kuishi muda mrefu kuliko wale ambao hawakusoma kazi hizo bali pia wanakuwa na namna nyingi za kukabiliana

² Katika makala haya riwaya ni kazi ya kubuni ya nathari ambayo matukio yake yamebuniwa. Matukio haya yanaweza kuwa yamechanganyika na matukio ya kweli pamoja na mazingira halisi yaliyopo katika jamii.

na mambo mbalimbali wanayokutana nayo katika maisha. Anabainisha kuwa kazi za bunilizi zinaweza kuleta mabadiliko makubwa katika maisha kwa kutoa mwelekeo kupitia uzoefu na mbinu mbadala za wahusika walio katika bunilizi husika. Kwa upande wao Kaufman na Libby (2012) wanaeleza kuwa kazi za bunilizi zinatusaidia kufikiri kama wahusika waliotumika katika kazi husika na/au hata kuwaza kufanya vitendo au kuwa na mawazo kama ya wahusika waliotumika katika kazi hizo. Si hayo tu, bali pia kazi za bunilizi hutusaidia kusafiri na kupata uzoefu wa watu wengine wenye usuli tofauti na wa kwetu, hutuwezesha kuona mambo kwa jicho la tofauti na hata kuona jinsi watu wengine wanavyopambana na changamoto wanazokutana nazo. Ni dhahiri kuwa wasomaji huweza kuelewa kwa undani kuhusu tabia mbalimbali za watu pamoja na yale wanayokutana nayo katika maisha yao ya kila siku. Naye Weedon (1997) anabainisha kuwa kutokana na kujifunza mambo mbalimbali, wasomaji wa bunilizi wanaweza wakaleta mabadiliko katika maisha yao binafsi na kwa jamii inayowazunguka. Hivyo, riwaya ikitumiwa vizuri inaweza kusawiri upya na/au kubadili kaida za jamii zinazowagandamiza wanawake ambazo ni vigumu kuzibadilisha kwa njia ya semina na makongamano (Ledbetter, 1996; Mosha, 2013). Kwa upande mwingine, Isaacs (2003) anasisitiza kuwa ni muhimu kuchunguza usawiri wa aina mbalimbali za unyanyasaji katika riwaya ili kujua ni mambo gani wasomaji wanaweza kujifunza kutoka katika bunilizi zinazotolewa hususan katika kukabiliana na suala la unyanyasaji. Katika makala haya jambo muhimu ni kubaini namna tunavyoweza kutumia riwaya za Kiswahili katika harakati za kupambana na tatizo la ubakaji katika jamii ya Tanzania.

2.0 Kiunzi cha Nadharia

Katika kuchunguza usawiri wa ubakaji katika riwaya teule za Kiswahili, makala haya yanaongozwa na nadharia ya Mahusiano ya Kijinsia na Madaraka. Nadharia hii inaonesha namna ambavyo tofauti za kibiolojia kati ya mwanamke na mwanamume zinavyotumika kusawiri jinsi mwanamke na mwanamume anavyotakiwa kuishi katika jamii (Connell, 1987). Connell anaeleza kuwa mwanamume anapewa kipaumbele katika jamii hususan katika kufanya maamuzi na kuongoza, jambo ambalo linaathiri hali ya mahusiano kati ya mwanamke na mwanamume kwa kiasi kikubwa. Connell (keshatajwa) anaendelea kufafanua kuwa uhusiano kati ya mwanamke na mwanamume umekuwa ukiangaliwa kwa kubainisha sifa zilizowekwa na jamii baina yao. Mathalani, mwanamume anategemewa kuonekana hodari, jasiri, anayefanya kazi za kipato na uwezo wa kuihudumia familia; wakati mwanamke anategemewa kuwa mnyenyeketu, kufanya kazi za nyumbani zisizoingiza kipato, kumhudumia mume wake na kulea watoto. Hali hii inajenga picha kuhusu mambo anayotakiwa kufanya mwanamume na mwanamke katika jamii. Mfumo huu umejenga mazingira ya kuwafanya wanaume waamini kuwa wana mamlaka ya kutoa amri na wanawake kuamini kuwa wanatakiwa kupokea amri kutoka kwa wanaume hususan katika suala zima la mahusiano. Akifafanua zaidi kuhusu hali ya mahusiano kati ya mwanamke na mwanamume, Mosha (2013) anaeleza kuwa ni hali inayokubalika kuwa

mwanamume ndiye anayefanya maamuzi katika jamii. Anafafanua kuwa mume ndiye anayeamu mke afanye kazi ya kipato (fedha) au la, jambo linalomfanya mwanamke akose nguvu za kiuchumi na kumtegemea mwanamume kwa kila kitu kinachohitaji fedha. Kutokana na hali hii vilongo vingi katika jamii vinamsawiri mwanamke kama mtu tegemezi anayelazimika kufuata amri na sheria zinazotolewa na mwanamume (Mosha, 2013). Mfumo dume unaotawala katika jamii nyingi za Kiafrika umejenga msingi wa mahusiano yasiyo sawa kijinsia; wanaume wakiwa ni wenyе maamuzi kuanzia katika matumizi ya rasilimali za familia, mahusiano ya kimapenzi na hata katika kupanga uzazi. Katika mahusiano haya wanawake wanazoezwa kuwa wanyenyekevu na wasiokuwa na maamuzi kwa waume zao, pamoja na kukosa uwezo wa kutawala mahusiano ya kimapenzi (Mugweni na wenzake, 2014).

Kwa upande mwingine Connell (2005) anadokeza kuwa ingawa kuna mabadiliko katika aina ya kazi zinazofanywa na wanaume na wanawake kutokana na mabadiliko ya kijamii, jamii zinazoongozwa na mfumo dume; bado miundo ya kimahusiano inatoa fursa kwa wanaume kuwa na mamlaka na nguvu zaidi kuliko wanawake. Pia, Connell anaongeza kuwa muundo wa mahusiano unaotengenezwa na jamii unaweza ama kutoa fursa kwa wanawake kufanya mambo mengi zaidi na hivyo kuondokana na utegemezi au kuwanyima fursa za kuweza kujitegemea. Kwa kutumia nadharia hii, makala haya yanalenga kuelewa ni kwa namna gani miundo ya kimahusiano na madaraka inachangia katika tatizo la ubakaji kama linavyosawiriwa katika riwaya teule za Kiswahili.

Aidha, makala haya yanaongozwa na kilongo cha ashiki ya kujamiihana ambacho kinachota kutoka katika nadharia za kibiolojia zinazoeleza kuwa kitendo cha kujamiihana kwa wanaume ni cha lazima. Hollway (1989) anafafanua kuwa ashiki ya kujamiihana ni chanzo cha wanaume kubaka wanawake kwa kuwa mahitaji ya kibiolojia yanawafanya wanaume washindwe kujizuia na hivyo kulazimika kuyakidhi. Kwa mujibu wa Gavey (2009) kilongo hiki kinabainisha kuwa mwanamume mwenye afya, ana ashiki kubwa ya kujamiihana, hivyo, kuwa na nguvu kubwa ambayo inatawala akili na uwezo wa kufikiri (Kitzinger & Powell, 1995). Katika kilongo hiki, wanawake wanalazimika kuhakikisha kuwa wanaume wanaridhiwa haja zao za kingono (Gavey, 2009; Reinholtz na wenzake, 1995).

Kwa upande wao, Kottler na Long (1997) wanaona kuwa haya ni mawazo yanayolenga kuhalalisha ubakaji kwa wanawake. Kwa hiyo, kilongo cha ashiki ya kujamiihana kinalenga kuwaondolea wanaume uwajibikaji katika matendo yao yahusuyo ngono kwa sababu hawana namna nyingine zaidi ya kuridhisha ashiki zao zenye nguvu. Aidha, Potts (2001) anaonya kuwa kumsawiri mwanamume kama mtu mwenye nguvu kubwa ya ashiki ya kujamiihana ambayo anashindwa kuitawala ni njia ya kumfanya mwanamume asiwajibike katika masuala ya ubakaji. Makala haya yanatumia kilongo hiki kuchunguza sababu zinazotolewa na waandishi wa riwaya teule za Kiswahili kuhusu suala la ubakaji.

3.0 Mbinu za Utafiti

Makala haya yanatokana na sampuli wakilishi ya riwaya sita za Kiswahili ambazo zimeteuliwa kutoka katika miaka ya miongo mitatu (1975 -2005). Jumla ya riwaya 20 za Kiswahili zenye maudhui yanayohusu unyanyasaji wa kingono ziliigizwa katika populesheni. Kupata data ya makala haya, usampulishaji lengwa ultumika kuteua riwaya sita zenye usawiri wa aina mbalimbali wa ubakaji. Riwaya zilizoteuliwa ni *Nyota ya Rehema* (Mohamed, 1976), *Wimbi la Huzuni*, (Kalindimya, 1988), *Dar es Salaam Usiku* (Mtobwa, 1990), *Almasi za Bandia* (Chachage, 1991), *Janga Sugu la Wazawa* (Ruhumbika, 2001). Riwaya hizi sita zilisomwa kwa makini na maeneo yaliyozungumzia ubakaji kwa masimulizi ya wazi au yasiyokuwa ya wazi yalinukuliwa. Kwa kuwa masimulizi yanajengwa kwa hadithi nzima - ili kupata mfululizo wa tukio husika, masimulizi yalichukuliwa kwa ujumla wake ili kuweza kufikia mahitimisho.

4.0 Usawiri wa Ubakaji katika Riwaya Teule za Kiswahili

Riwaya za Kiswahili zinazeleza ubakaji kuwa unasababishwa na ashiki ya kujamiihana yenye nguvu kubwa ambayo baadhi ya wanaume wanashindwa kuizua. Mfano ufuataao kutoka katika riwaya ya *Nyota ya Rehema*, unazeleza namna ambavyo Bwana Mansuri, mwanamume mwenye mke na mtoto mmoja anavyojaribu kumbaka Rehema (mtumishi wa kazi za ndani) mkewe alipokuwa kazini:

“Njoo huku,” alimsikia akisema. Rehema alikwenda. Alimwona kamshika mkono na akaingia naye katika chumba cha kulala. ...
Kutahamaki, Rehema alimwona Mansuri akimpandisha kitandani. ...
“Ngojea kwanza bwana Mansuri,” ... “unataka kufanya nini?”
“Usijifanye mtoto, Rehema, unajua kuwa mimi nakupenda,” alisema Mansuri, sauti yake ilikuwa imebadilika. “Hebu kwanza, bwana Mansuri, mimi si ...sitaki ...” ... Aliyekuwa akisema naye alikuwa keshaaingia katika daraja ya uhayawani (Mohamed, 1976, uk. 64).

Kulingana na nukuu iliyotolewa, Mansuri ameshikwa na ashiki kubwa ya kujamiihana kiasi cha kushindwa kumweleza Rehema jambo alilomwitia, badala yake anamshika mkono na kumpeleka chumbani kwake na kumtupa kitandani ili aweze kutimiza azma yake. Kutoakana na nukuu hiyo, inaweza kuelezwa kuwa Mansuri haelewi alilokuwa anafanya kutoakana na ashiki kubwa ya kujamiihana aliyokuwa nayo. Jewkes na wenzake (2006) wanaeleza kuwa kisingizio cha kuwa ashiki ya kujamiihana haitawaliki kinaweza kutumiwa kuhalalisha ubakaji. Usawiri wa aina hii, unaweza kutumika kumtetea mwanamume anayebaka ili asiadhibiwe kwa sababu analazimika kuridhia matakwa haya muhimu ya kibiolojia. Aidha, ingawa suala la tofauti za kimahusiano na kiuchumi (baba/mtoto na mwajiri/mwajiriwa) linachangia halijitokezi katika masilimulizi.

Kwa upande mwingine, Rehema hakuwa tayari kujamiiana na bosi wake bali alipambana naye kama nukuu ifuatayo inavyoeleza:

Rehema alitumia uwezo wake wa mwisho, nao ni kuzamisha meno yake katika bega la Mansuri! Mansuri aligutuka kwa maumivu na kujitupa upande wa pili, Rehema akapata nafasi ya kuponyoka. ... Kisha akageuka na kutoka mbio mpaka chumbani kwa mtoto, akakomea mlango kwa pete, na kujitupa juu ya kiti huku akilia. (Mohamed, 1976: 65)

Katika nukuu hii, mwandishi anamwelezea Rehema kama msichana jasiri aliyefanikiwa kupambana na bosi wake aliyetaka kumbaka, ingawa bosi wake tayari ashiki ya kujamiiana ilikuwa haizuiliki. Hapa mwandishi amemsawiri Rehema kama msichana aliyweweza kuyashinda mawazo zoelevu kuwa msichana/mwanamke hawezi kufanya jambo lolote anapotaka kubakwa. Pia, mwandishi anawajengea uwezo wasichana/wanawake kuamini kuwa si lazima kukubali kujamiiana endapo mmoja hajaridhia.

Hata hivyo, badala ya kuendeleza msimamo huu wa kijasiri, mwandishi anasawiri kitendo cha kijasiri alichofanya Rehema kuwa hakikubaliki kwa kuwa Rehema amesababisha maumivu makali kwa bosi wake. Hii inaonesha kuwa kitendo alichofanya, kukataa kujamiiana na bosi wake si sahihi na Mansuri alikuwa na haki ya kujamiiana na Rehema. Masimulizi yanavyoendelea, mwandishi anamsawiri upya Rehema na analazimika kwenda kumwomba Mansuri (bosi wake) msamaha kwa kumsababishia maumivu. Tofauti na tukio la awali ambapo Mansuri alijaribu kumbaka Rehema, hapa mwandishi anamsawiri Rehema kuwa alimfuata bosi wake chumbani na hivyo kumshawishi kufanya naye mapenzi. Hapa Mansuri anapata nafasi ya kutimiza haja yake ya kujamiiana na Rehema kama nukuu hii inavyodhahirisha:

Rozi alipokuwa katoka ... Rehema alielekea upande wa chumba alicholala Mansuri. ... Akaingia ndani na kumkuta Mansuri kakaa juu ya kitanda... Mansuri alimtzama Rehema pasi na kumsemesha lolote. ... Rehema, katika hali ya woga na kubanwa na hisia ngeni asiyoijua alisimama mbele yake kama mpumbavu ... tone za machozi zikichungulia katika pembe za macho yake. Mansuri ... akanyanyuka na kumshika mkono Rehema, kimya kimya, pole pole, na kumpandisha kitandani, kwani alijua Rehema alitaka nini. (Mohamed, 1976: 73-74)

Ukichunguza kwa makini nukuu hizi, unaona kuwa nukuu ya awali mwandishi anamsawiri mwanamke kama mtu jasiri anayeweza kupambana na ubakaji. Usawiri wa aina hii unatoa matumaini kwa wanawake na wale ambao wanapambana na vitendo vyta ubakaji. Lakini nukuu ya pili inaonesha kuwa

ubakaji ni kitendo cha kawaida na hapa Bwana Mwansuri anaonekana kuwa hana makosa kwani Rehema ameridhia mapendekezo ya kufanya ngono bila kulazimishwa.

Kwa upande mwingine, tatizo la ubakaji katika riwaya za Kiswahili linaoneshwa kuwa ni matokeo ya tofauti za kimadaraka ambapo wanaume wanapata yale wanayotaka kunatokana na mfumo wa jamii unaokubali ugandamizaji dhidi ya wanawake (Ferraro, 1996). Wanaufeministi wanafafanua kuwa ubakaji siyo kosa linalotokana na ukosefu wa utashi bali ni kitendo cha kikatili kinachotumiwa na wanaume ili kuwatawala na kuwanyamazisha wanawake (Scully na Marolla, 1993). Ukweli huu unaonekana katika riwaya ya *Wimbi la Huzuni* ya Kalindimya (1988), ambapo mwandishi anaonesha namna wanaume wakatili wanavyofanya vitendo vyao bila kuadhibiwa na mtu yejote. Kalindimya anaeleza namna msichana wa miaka 11 (Seya) aliyekimbia kutoka katika kituo cha kulea watoto yatima anavyobakwa kikatili na kikundi cha wanaume:

Kutenda unyama limekuwa tukio la kawaida. Ni matendo ambayo watu wanatenda na kujivunia. Kila wanapofanya majaribio ya uovu na kufanikiwa, walitenda wanatenda tena na tena, na hata imegeuka sehemu ya maisha yao ya kila siku. Seya wa watu, kinyume na utashi wake wakamtenda kinyama. Si mmoja la hasha, ila msululu wa wanaume, wenye uchu na waliodhamiria. ... Kwa uchungu wa maumivu, Seya akazimia na hata alipozinduka, alijikuta yupo kwenye hospitali ya Mwananyamala (Kalindimya, 1988:14-15).

Katika aya zilizonukuliwa hapo juu, utamaduni wa kutenda maovu umeoneshwa kama sababu ya wanaume kuwa wakatili kwa wanawake. Ingawa mwandishi ameonesha jamii kuvumilia ukatili, anaonesha pia kuwa wanaume wana kiu ya kujamiihana. Aina hizi mbili za vilongo – utamaduni wa ukatili na ashiki ya kujamiihana, vimesawiriwa kwa pamoja na vinafanya kazi kwa pamoja kama njia ya kuhalalisha ukatili kwa wanawake. Vilongo hivi vinakamilishana – wakati ukatili ni jambo la kiutamaduni, ubakaji ni jambo la kibiolojia na kwa hiyo ni la kawaida. Kwa minajili hii, wanaume wanastahili kusamehewa kutokana na ukatili wao ikiwa ni pamoja na ubakaji.

Mifano zaidi kuhusu ashiki ya kujamiihana tunaipata katika riwaya ya *Dar es Salaam Usiku* (Mtobwa, 1990). Katika riwaya hii mwandishi anaeleza kuwa wanaume wanatumia nguvu za kiuchumi katika kuwarubuni wasichana wadogo ili kutimiza haja zao za kingono. Mtobwa anaeleza namna mwanamume mmoja alivyofanikiwa kumbaka Rukia msichana wa miaka 11 aliyejewa anatafuta chakula kwenye mabaa baada ya kutelekezwa na mama yake:

Aliyajua macho ya msichana anayetaka mwanamume na alijua anayemlilia. Ya Rukia aliona "yakimlilia" kabisa. ... Aliwapenda

hawa kwa sababu za kiuchumi. ...“Twende zetu Nyamanoro, nina chumba changu.” “Mia mbili hazitoshi.” “Mia tatu?” “Hazitoshi. Bwana wangu ananipa mia tano kila asubuhi.” Bwana huyu alishangaa. Mtoto huyu ameijulia wapi pesa kiasi hicho? ... Bia ya pili aliinywa haraka kuliko mwenyeji wake. Mwenyeji wake aliyaona hayo akamshawishi kuendelea kunywa haraka zaidi. ... Ya tano hakumbuki kama aliinywa. ... Alikuwa taabani. Hakuiona hata shilingi kati ya pesa ambazo alikuwa tayari amepewa na bwana huyo. (Mtobwa, 1990: 56-57)

Igawa katika riwaya hii, Mtobwa ameonesha ubakaji kama njia ya baadhi ya wanaume kutimiza azma zao za kingono, anamsawiri Rukia kama malaya mzoefu na hivyo kuweza kumwita mwanamume kwa macho yake na hata kuwa na uzoefu wa kujadiliana kiasi cha fedha. Katika nukuu iliyotolewa, mwandishi anamlamu Rukia kwa kukubali kunywa pombe mpaka akalewa na hivyo kushindwa kujua kilichoendelea. Aidha, katika riwaya hii Mtobwa anamlamu mama yake Rukia kwa kumtelekeza mtoto akiwa na umri mdogo. Akina mama kulaumiwa pale watoto wanapopata matatizo imeelezwa pia na watafiti wengine. Mathalani, Jewkes na wenzake (2006) wanabainisha kuwa, katika nchi ya Afrika Kusini wanawake wanalaumiwa kwa kuwaacha watoto wa kike wenyewe jambo linalotoa nafasi kwa baadhi ya wanaume kuwabaka. Katika riwaya ya *Dar es Salaam Usiku* badala ya mwandishi kukemea na kumlaani mhusika mwanamume anayempa mtoto mdogo pombe na kisha kumbaka, anamlamu mama yake aliyemtelekeza. Usawiri wa namna hii unawabebesha lawama wanawake kwa kuwaona kuwa hawawezi kutimiza vyema jukumu lao la ulezi lakini wanaume hawaonekani kuwajibishwa kwa kufanya vitendo vya kinyama ambavyo havikubalika katika jamii.

Mfano mwingine ambapo ashiki za kujamiihana zinatumika kusawiri ubakaji ni katika riwaya ya *Janga Sugu la Wazawa* (Ruhumbika, 2001). Katika riwaya hii Ruhumbika anamwelezea Bugonoka, msichana aliyeveza kupambana na Padre Joni aliyetaka kumbaka nyumbani kwake alipokwenda kumtembelea. Padre Joni alikuwa anamtembelea Bugonoka mara kwa mara kwa madai ya kumfundisha Neno la Mungu. Siku alipojaribu kumbaka, Padre Joni alieleza wazi kuwa lengo hasa la kwenda kumtembelea halikuwa kumfundisha neno la Mungu bali lilikuwa ni kuwa na mahusiano ya kimapenzi. Bugonoka alipokataa maombi yake, Padre Joni hakuwa tayari kusikiliza majibu ya Bugonoka na hivyo kujaribu kumbaka kama nukuu ifuatayo inavyoeleza:

Alipotaka kupita pale huyo Padre alipokuwa amekaa ili atoke nje, Padre Joni akamdaka mkono, na hapo hapo akamvuta hadi kwenye mlango, akafunga mlango na kubana komea la mlango. Halafu, kwa mikono yake yote miwili, akamshika huyo mwanamke mbichi aliyekuwa anamtia wazimu hivyo na kumbania kifuani kwake, na

kusikia joto la matiti yake, huku mkia wake uliokwisha vimbiana kama kifutu anayetaka kuuma mtu unatafuta mapaja laini ya huyo kigoli (Ruhumbika, 2001: 95).

Katika nukuu hii, mwandishi amemsawiri Padre Joni kushindwa kujitawala hivyo kutaka kumbaka Bugonoka. Ingawa Padre Joni alimweleza Bugonoka kuwa alikuja hapo kwa kuwa alimpenda, mwandishi anaweka wazi katika masimulizi kuwa alihamishiwa hapo kutokana na tabia zake za unyanyasaji alizooonesha katika parokia aliopangiwa awali. Mwandishi analaumu Kanisa Katoliki kwa tabia zake za kutowaadhibu mapadre wanaowanyanya wanawake na badala yake wanawahamishia sehemu nyingine.

Katika masimulizi, Ruhumbika anaeleza kuwa Bugonoka alisifiwa sana kutokana na ujasiri wake wa kutomruhusu mwanamume kumchezea. Mwandishi anazidi kueleza kuwa wanajamii wengi walijadili namna Bugonoka alivyoweza kupambana na mwanamume aliyezoea kuwapata wanawake kwa nguvu na kuhitimisha kuwa inawezekana wanawake kuwazuia wanaume wanaotaka kuwabaka. Ni wazi kuwa usawiri wa aina hii unatoa mwanga kuwa kuna uwezekano wa kuwa na vilongo tofauti kuhusu ubakaji ambavyo vinatoa nafasi kwa wanawake kujilinda na kukataa pale ambapo hawataki kujamiihana.

Kwa mshangao mkubwa, Ruhumbika anavyoendelea na masimulizi katika riwaya yake, anatoa usawiri kinzani kwa Bugonoka kwa kumwonesha kuwa kiutamaduni ni mwanamke mbaya aliyetaka kuua. Kutokana na kitendo hiki cha kikatili alichotaka kumfanyia mwanamume aliyetaka tu kujamiihana naye, Bugonoka anauawa kinyama na sehemu zake za siri anapelekewa Padre Joni. Padre Joni ndiye aliyetuma watu kumwua Bugonoka na wakati huo alikuwa amebadili dini na kuwa Mwislamu, Shehe na Mganga wa Kienyeje. Kulingana na masilimuzi, kuuawa kwa Bugonoka ilikuwa ni adhabu kwa kumzuia mwanamume aliyetaka kumbaka. Masimulizi haya yanaonesha kuwa wanawake wanaojaribu kuwazuia wanaume wanaotaka kutimiza haja zao za kingono wanakwenda kinyume na vilongo vya kiutamaduni vinavyowaelekeza wanawake kuhakikisha kuwa wanaume wanaridhiwa haja zao za kingono (Gavey, 2009; Reinholtz na wenzake, 1995).

Haijalishi kuwa mwandishi alikuwa ana nia gani, aina hii ya usawiri inalenga kuwanyamazisha na kuwahimiza wanawake wasithubutu kупingana na wanaume wanaotaka kuwabaka, kwani kufanya hivyo kutawasababishia unyanyasaji mkubwa zaidi. Lakini jambo muhimu zaidi, usawiri wa aina hii wa kumwadhibu mwanamke anayejilinda au kukataa kumtimizia mwanamume haja za kingono una madhara zaidi kwa jamii kwani unashadidia tabia zinazowataka wanawake kuwaridhisha wanaume kingono hata pale ambapo hawako tayari.

Ukweli huu wa kuwaadhibu wanawake wanaokataa kuridhia haja za wanaume wenye ashiki kali ya kujamiihana unaelezwa kwa undani na Mohamed (1977) katika riwaya ya *Asali Chungu*. Katika riwaya hii Mohamed anasimulia namna Zuberi alivyombaka Semeni. Semeni alikuwa ni mtoto yatima aliyetoka kijijini na kuwa mfanyakazi wa ndani nyumbani kwa Zuberi. Awali katika masimulizi yake, mwandishi anaeleza namna Semeni alivyomghadhibisha Zuberi baada ya kumkataa alipomtaka wawe na mahusiano ya kingono. Mwandishi anaeleza kuwa majibu ya Semeni ya kumkataa Zuberi siyo tu yalimpandisha hasira na kumdhalilisha, bali pia yalizidisha hamu ya Zuberi kuhakikisha kuwa anampata Semeni, kama nukuu hii inavyoonesha:

Kweli sina haki ya kukataa matakwa yako lakini ... jambo ulitakalo ni zito kwangu. Nakuomba uniwie radhi. Nisamehe sana Bwana. ...
Mimi nifanye mtumishi wako tu. Nione kama nitakayekunajisi. ...
Kesho tu jambo hili litakuwa nje, nalo litaharibu jina lako kuwa Bwana, mwenye enzi yake, kenda na kitumishi chake. Maneno hayo yalimpaka tope Zuberi. Undani wake alishautoa; fedheha ameipata; na Semeni kamkosa. ... Kwa mara ya mwanzo kakutana na machungu ya kukataliwa – kukataliwa na mtu duni kabisa kwake. Hiyo ndiyo asili ya kupanda mori, akaona atende lolote mpaka amtie makuchani Semeni (Mohamed, 1977: 17).

Tukichunguza kwa makini nukuu hii tunagundua kuwa kitendo cha Semeni kukataa maombi ya bosí wake ya kuwa na mahusiano ya kimpenzi ni kitendo ambacho hakikutegemewa na Zuberi na hakuwa tayari kufanyiwa hivyo na mtu ambaye yeye alimwona kuwa hana thamani. Hali hii ilimfanya Zuberi kuazimia kufanya lolote ili kuweza kujamiihana na Semeni.

Kwa kuzingatia vilongo zoeleka vya kijamii kuhusu mwanamke anavyotakiwa kumridhisha mwanamume kingono (Gavey, 2009), mwandishi anaeleza namna Bwana Zuberi alivyomtumia Biti Daudi, mwanamke mtu mzima kumshawishi Semeni akubali maombi yake:

Biti Daudi akamrai akubali ombi lake. ... "Mwanangu, kuna waliolala masikini wakaamka matajiri. Mjukuu wangu, unajivunjia riziki yako 'ivyo, haaaya. ... Kuna walionunuliwa nyumba mama, waliofuliwa vyombo vya dhahabu kochokocho; kuna walioandikwa vikata na mashamba ya fahari. ... Basi iweje mama, bwana kama huyu kukutaka wewe usimjali. Huoni kwamba unajiharibia hivyo? Eee mwana, unajivunjia riziki zako we! Ee haaaya!" Biti Daudi aliona labda amenasishika; lakini wapi! Semeni aling'ang'ania sitara. ... Jambo hilo lilizidi kumghadhabisha Zuberi. (Mohamed, 1977: 17-18)

Kilongo cha ashiki za kujamiihana na uwezo wa kiuchumi vinatumwiwa sambamba na wanaume katika kukidhi haja zao za kingono (Hollway, 1989). Hollway anaeleza kuwa uwezo wa kiuchumi unawapa wanaume nguvu za kuhakikisha kuwa haja zao za kingono zinatimizwa kwa kuwawezesha kulipia endapo inahitajika. Kwa uelewa huu, Biti Daudi katika nukuu iliyotolewa hapo juu anamwona Semeni kama msichana mwenye bahati lakini hajui anachotaka kufanyiwa na bosi wake na hivyo msimamo wake unapingana na vilongo zoeleka vya mahusiano kati ya mwanamke na mwanamume katika jamii ambapo kwa kawaida mwanamke anakubaliana na mapendekezo yanayotolewa na mwanamume hususan katika mahusiano ya kingono (Gavey, 2009). Kulingana na maoni ya Biti Daudi, msimamo wa Semeni hauendani na matarajio ya walio wengi, msichana maskini kumkataa mwanamume mwenye heshima zake tena tajiri katika jamii. Kwa hiyo, kukataa kwake kunachukuliwa kama kuna matatizo na tena hakukubaliki katika jamii.

Aidha, hali ya wanawake kutothaminiwa mawazo yao pale wanapokataa maombi ya mahusiano ya kimapenzi, kunaelezwa na wanaufeministi kuwa ni kutokana na baadhi ya wanaume kuamini kuwa wanawake wanalazimika kuwardidhia haja zao; lakini pia, baadhi ya wanawake kuhimizwa kufanya hivyo na pale wanawake wachache wanapokataa inaonekana kuwa wamekwenda kinyume na matarajio ya jamii na hivyo kujikuta wanabakwa na wanaume waliowakatalia na/au kuadhibiwa (Scully & Marolla, 1993). Ukweli wa jambo hili umeelezwa na Mohamed baadaye katika riwaya hii ya *Asali Chungu*. Mwandishi anaeleza kuwa Zuberi alipoona kuwa Semeni amemkataa hata baada ya kutumia mbinu za kiuchumi kuitia Biti Daudi, aliamua kuweka mkakati wa kumbaka usiku akiwa amelala. Mikakati aliywewka ni pamoja na kununua dawa ya usingizi ya kumfanya Semeni asijitambue. Mbinu aliyotumia Zuberi inaelezwa pia na Jewkes na wenzake (2006) kuwa kwa kawaida wanaume wanaowabaka watoto huwa wanajiandaa kuhakikisha kuwa hawawezi kukamatwa. Mwandishi anaeleza kuwa baada ya Zuberi kufanikisha azma yake anajitapa kuwa pamoja na kukataliwa ameweza kumpata kirahisi kabisa Semeni.

Madhara ya kubakwa kama yanavyoolezwa na mwandishi katika riwaya hii yanafanana na yale yanayoainishwa katika tafiti mbalimbali za kifeministi zinazoeleza kuwa ubakaji una madhara ya muda mrefu katika maisha ya wanawake. Mathalan, Koss na wenzake (1994) wanaeleza kuwa madhara ya kubakwa ni pamoja na kupata mimba zisizotarajiwa, msongo wa mawazo na wakati mwingine kujiua. Katika riwaya ya *Asali Chungu*, mwandishi anaeleza kuwa Semeni aliteseka sana baada ya kubakwa na Zuberi. Semeni alikimbia siku iliyofuata baada ya kugundua kuwa alibakwa. Miezi michache baadaye aligundua kuwa alipata mimba iliyotokana na kubakwa na alijifungua mtoto wa kiume. Maisha yalikuwa magumu sana kwa sababu alikuwa hana kazi. Hali hii ilimfanya kuwa mlevi na hata kujihusisha na umalaya. Mwisho, Semeni alijiua baada ya kugombana na dada aliyekuwa anaishi naye kwa sababu alimchukua mpenzi wake.

Haya yaliyotokea katika maisha ya Semeni yanadhihirisha maneno aliyoambwa na Biti Daudi, ‘Huoni kwamba unajiharibia hivyo? Eee mwana, unajivunja riziki zako we! Ee haaaya!’ (Mohamed, 1977:17).

Kwa kiasi kikubwa usawiri wa aina hii unashadidia vilongo zoleka vya jamii kuwa mwanamke hawezi kukataa mapendekezo ya kimahusiano ya mwanamume na akijaribu kufanya hivyo atapata madhara makubwa katika maisha yake.

Ingawa masimulizi ya kina yametolewa kuhusu mambo yaliyotokea kwa Semeni baada ya kubakwa, hakuna taarifa zilizotolewa kuhusu Zuberi baada ya kitendo hiki cha kinyama. Hakika huku kumakinikia maisha ya mhanga kwa kuonesha namna alivyopata mteso huenda ni mbini ambayo inaweza kuchukuliwa kama njia ya kuhalalisha vitendo vya kinyanyasaji kwa wanawake na kuwahimiza wanawake kukubaliana na mapendekezo ya wanaume ya kimahusiano. Vilevile, vitendo vya kinyanyasaji vinaoneshwa kama ni vya kawaida na havina athari yoyote kwa wanaume lakini vina madhara makubwa kwa wanawake na hasa kwa Semeni ambaye mwandishi anaonesha kuwa anahuksika zaidi na yaliyomtokea kwa kujaribu kukataa mapendekezo ya mahusiano kutoka kwa mtu tajiri. Adha, bila kujali lengo na nia ya mwandishi kusawiri aina hii ya ubakaji, hii inaonesha madhara ya kwenda kinyume na yale yanayokubalika katika jamii. Hakika, mawazo ya baadhi ya wanaume kudhani kuwa wanawake ni chombo chao cha starehe na uhalali wao wa kutumia nguvu wanapokataliwa maombi yao yanawekwa wazi katika utafiti wa Scully na Moralla (1993) unaoeleza ni kwa nini wanaume wanawabaka wanawake. Katika utafiti wao waliwahoji wanaume 144 waliobaka kupata maoni yao ni kwa nini walibaka. Mwanamume mmoja ambaye alimwua mwanamke aliyekataa mapendekezo yake ya kuwa na mahusiano alisema:

Kubaka ni haki ya mwanamume. Kama mwanamke hataki, mwanamume ana haki ya kumbaka. Mwanamke hana haki ya kusema hapana. Wanawake wameumbwa kwa ajili ya kuwardhisha wanaume. Huo ndio wajibu wa kwanza wa wanawake. Wanawake wengine wako radhi kupigwa, lakini mwishoni wanakubali, ndiyo kazi waliyopewa - kuwardhisha wanaume (Scully na Moralla, 1993: 42).

Kwa mtazamo kama huu unaowapa wanaume uhuru wa mahusiano, Zuberi haoni ni kwa nini asitumie nguvu kupata kitu anachofikiri ni haki yake na mwandishi hakuonesha usawiri mbadala kupinga mtazamo huu wa Zuberi. Kwa hiyo, ni muhimu kuhoji si tu mtazamo kuhusu wanawake kuwa mali ya wanaume lakini pia mfumo wa jamii unaolea mtazamo huu na kuuendeleza.

Kwa upande mwingine, tafiti mbalimbali zinabainisha kuwa ubakaji ni tatizo linalowakumba wanawake wa kila kada. Kuanzia watoto ambao hawakupata

nafasi ya kupata elimu ya juu kama vile Semeni na Rehema mpaka wale wenye elimu ya chuo kikuu. Chachage (1991) katika riwaya ya *Almasi za Bandia* anaeleza namna ambavyo Patricia, mwanafunzi wa chuo kikuu, anavyobakwa na Merton, mwanafunzi mwenzake. Mwandishi anaeleza kuwa Merton alifanikiwa kumbaka Patricia baada ya kumkaribisha nyumbani kwa rafiki yake Ayuka. Merton alipanga na rafiki yake Ayuka kwa sababu alikuwa anaishi na mkewe kwa hiyo ilikuwa vigumu kumkaribisha nyumbani kwake. Merton alikuwa amemweleza Ayuka nia yake ya kujamiihana na Patricia siku nyingi, walipofanikiwa kumkaribisha Patricia nyumbani kwake, Ayuka aliwaacha na kufunga mlango akidai kuwa anakwenda kununua vinywaji. Hii ilitoa nafasi kwa Merton kuweza kutimiza lengo lake kama Chachage anavyoeleza:

Kwa sauti ya kukoroma iliyoathirika na ashiki za kihayawani, Merton aliongea huku kaisogeza mikono yake kwa Patricia. ... Patricia alisimama haraka na kukimbilia mlangoni. ... Alijaribu kukizungusha kitasa cha mlango. ... Kwa sauti kali ya kutetemeka alimwamuru Merton, "Usinisogele! Ukinisogele tu nitapiga kelele!" Merton alicheka kifedhuli na kumjibu, "Unapoteza wakati wako bure! Hakuna atakayekuamini." ... Patricia alitamani apige yowe, lakini sauti ilimhaini akashindwa kufanya hivyo. ... Alipofikiri juu ya aibu ambayo angeipata pindi watu wangeingia pale baada ya kusikia yowe, na kisha wakakosa kuamini ambacho angewaeleza. ... Sasa Merton alikuwa amefaulu ... aliiivuta chupi ya yule msichana na kuichanilia mbali. ... [Patricia] akaendelea kupigana ... Kwa Merton, majaribio ya Patricia kujikwamua pale, hazikuwa dalili za kukataa, bali kujibaraguza kwa kike. Kama angekuwa amekataa, basi angepiga kelele (Chachage, 1991: 70-71).

Walby na wenzake (1983) wanafafanua kuwa mara nyingi ubakaji unapangwa ikiwa ni pamoja na kuandaa eneo la kufanya tukio hilo na kumbainisha mhanga. Unyanyapaa wa jamii kuhusu ubakaji umebainishwa na mwandishi katika nukuu ya pili kuwa unasaidia katika kuhalalisha unyanyasaji wa kingono kwa kumnyamazisha mhanga. Unyanyapaa unawafanya wanaume wanyanyasaji kuendelea kuwanyanya wanawake na unahimiza wahanga kuvumilia vitendo hivyo vya kikatili kwani hata mhanga akipiga kelele kuwa anabakwa, hakuna atakayemwamini. Hali hii imejibainisha wazi katika mazungumzo wakati Merton alipomwambia Patricia, "Unapoteza wakati wako bure! Hakuna atakayekuamini."

Mwanzoni mwandishi alieleza kuwa Merton alimweleza Yakini (rafiki ya Merton na Patricia) kuwa Patrcia ni mpenzi wake. Yakini alijua si kweli na akapanga kumwuliza Patricia lakini hakuwahi kumwuliza. Patricia alipomweleza Yakini kuwa alibakwa na Merton, Yakini alijuta kucheleva kumtahadharisha majigambo ya Merton. Baada ya Merton kumbaka Patricia, alianza kujigamba kwa rafiki zake kuwa ilikuwa rahisi sana kumpata Patricia na kujamiihana naye. Kwa mshangao

Yakini alimwambia: "Unadhani sisi hatujui kwamba ulimnajisi Patricia kwa nguvu nyumbani kwa ... Ayuka?" (Chachage, 1991: 75).

Merton alikasirika sana na akataka kumpiga Yakini lakini marafiki zake walimzuia. Hata hivyo, Merton alisisitiza kuwa siku moja Yakini atajua yeze ni mtu muhimu. Miaka mingi baadaye Merton alishambuliwa na watu wasiojulikana na kuumizwa vibaya. Merton alimhusisha Yakini na tuhuma hizo. Yakini alikamatwa na polisi na kuteswa sana, ingawa alikuwa hajui lolote kuhusu mashambulizi hayo. Baadaye kabisa, Merton akaeleza kuwa mashambulizi hayo yalipangwa na Inspekte Gordon kwa sababu za kibiashara lakini akaamua kumsingizia Yakini kwa sababu waligombana kwa ajili ya Patricia. Katika masimulizi inaonekana wazi kuwa Merton alilipiza kisasi kwa kuwa Yakini aliweka wazi maovu yake (kumbaka Patricia) jambo alilojua ni siri. Kwa hiyo, katika riwaya hii mwandishi analenga kuonesha changamoto fungamanishi juu ya suala la ubakaji katika jamii ya Tanzania ikiwa ni pamoja na kumwadhibu anayejaribu kufichua uovu unaofanywa na wabakaji.

5.0 Hitimisho

Makala haya yameangazia usawiri wa ubakaji katika riwaya sita za Kiswahili za vipindi tofauti. Katika riwaya zilizoteuliwa, ubakaji umedhihirika kuwa ni unyanyasaji unaotumia mbinu fungamani. Katika masimulizi ya waandishi wa riwaya teule, sababu kubwa inayochochea aina hii ya unyanyasaji ni ashiki za kujamiihana, nguvu za kiuchumi walizonazo wanaume na unyanyapaa wa jamii. Waandishi wa riwaya teule wameangazia kwa undani yale yanayomhusu mhanga na hata wakati mwingine kuonesha kuwa mbakaji hana makosa. Usawiri wa aina hii unaweza ama ukakwamisha juhudzi za kupambana na aina hii ya unyanyasaji au kuendeleza vitendo hivi vya unyanyasaji. Aidha, baadhi ya waandishi wamesawiri mtazamo zoeleka unaochochea unyanyasaji wa wanawake bila kukosoa mtazamo huo. Mitazamo hiyo ni ile inayochochea wanawake kuwanyenyeka wanaume na kutii kila jambo bila kuangalia madhara wanayoweza kupata wanawake wanapofanya hivyo. Kwa kufanya hivyo, waandishi wanachochea mfumo unaowanyanya wanawake na hata kuwanyima haki zao za msingi ikiwa ni pamoja na kutawala mili yao.

Katika harakati za kukomesha ubakaji, riwaya za Kiswahili zinaweza kuchangia kwa kusawiri vilongo mbadala ambavyo vitawasaidia wanajamii kuwa na mtazamo na mawazo tofauti kuhusu suala hili. Kwa mfano, waandishi wanaweza kutumia vilongo vya haki za binadamu na maadili mema ya jamii katika kukemea unyanyasaji huu. Usawiri wa aina hii unaweza kubadili mawazo ambayo wanajamii walikuwa nayo awali kuwa ubakaji ni jambo la kawaida na haliwezi kuepukika.

Aidha, kutokana na waandishi kuelewa madhara makubwa yanayotokana na ubakaji, wanaweza kubainisha mbinu zinazoweza kutumiwa na jamii katika

kukomesha unyanyasaji huu. Mojawapo ya mbinu wanazoweza kutumia waandishi ni kukosoa vilongo zoleka vinavyoshadidia ubakaji pamoja na kubainisha mbinu zitakazowasaidia wanawake kuondokana na unyanyasaji huu. Aidha, wanawake wanaweza kutumia mbinu hizo kubadili nafasi waliyopewa na jamii ya kunyanyaswa na wanaume hususan katika eneo hili la mahusiano.

Pia, waandishi wanaweza kutoa mchango wao kwa kuhakiki kwa jicho pevu mfumo dume unaoendeleza unyanyasaji wa wanawake katika jamii, kwa kuonesha unavyoendeleza unyanyasaji. Hii itasaidia wanajamii kuelewa kwa undani tabia zinazolea na kupalilia ubakaji. Vilevile, kuchunguza mfumo wa jamii kutasaidia kugundua namna tatizo hili linavyopewa nguvu na jamii. Jamii ikielewa ni kwa namna gani inahusika na suala zima la ubakaji na endapo itakuwa tayari kukomesha unyanyasaji huo, basi itasaidia katika kutafuta mbinu za kuondokana na mfumo huo. Kwa kufanya hivyo, riwaya zinaweza pia kubainisha namna kila mwanajamii anavyoweza kuwa mhanga kwa kuonesha namna wanavyoweza kuhusika katika ubakaji kwa kuwa watenda au watendwa. Kwa njia hii, riwaya zitasaidia kuelimisha jamii kuhusu suala hili na kuionya jamii kuhusu madhara ya kuendelea kushadidia mawazo yanayoendeleza unyanyasaji kwa wanawake.

Marejeleo

- Antonowicz, L. (2010). *Too often in silence: A report on school-based violence in West and Central Africa*. Retrieved from <http://www.e4conference.org/wp-content/uploads/2010/04/14en.pdf>
- Chachage, C. S. L. (1991). *Almasi za Bandia*. Dar es Salaam, Tanzania: Dar es Salaam University Press.
- Connell, R. W. (1987). *Gender and Power*. Sydney, Australia: Allen and Unwin.
- Connell, R. W. (2005). Globalization, Imperialism, and Masculinities. Katika *Handbook of studies on men & masculinities*, M. S. Kimmel, J. Hearn, and R. W. Connell (Wahariri). Thousand Oaks, CA: Sage.
- Ferraro, K. J. (1996). The Dance of Dependency: A Genealogy of Domestic Violence Discourses. *Hypatia*, 11(4), 77-91.
- Gavey, N. (2009). Fighting Rape. In R. J. Heberle & V. Grace (Eds.), *Theorizing sexual violence* (uk. 96-124). New York, NY: Routledge.
- Hayakawa, S. I. (1990). *Language in Thought and Action*. New York: Harcourt Brace
- Hollway, W. (1989). *Subjectivity and Method in Psychology: Gender, Meaning and Science*. London, England: Sage.
- Isaacs, K. T. (2003). Reality Check: A look at the disturbing growth of violence in books for teens. *School Library Journal*, 49(10), 50-51.
- Jewkes, R., Dunkle, K., Koss, M. P., Levin, J. B. (2006). Rape Perpetration by young, Rural South African Men: Prevalence, patterns and risk factors. *Social Science & Medicine*, 63(11), 2949-2961.

- Kalindimya, J. E. (1988). *Wimbi la Huzuni*. Dar es Salaam, Tanzania: Tajack Industries Ltd.
- Kaufman, G. F., & Libby, L. K. (2012). Changing Beliefs and Behavior Through Experience Taking. *Journal of Personality and Social Psychology*, 103(1), 1-19.
- Kitzinger, C., & Powell, D. (1995). Engendering Infidelity: Essentialist and Social Constructionist Readings of a Story completion Task. *Feminism & Psychology*, 5(3), 345-372.
- Koss, M. P., Goodman, L. A., Browne, A., Fitzgerald, (1994). *No Safe Haven: Male Violence Against Women at Home, at work, and in the Community*. Washington, DC: American Psychological Association.
- Kottler, A., & Long, C. (1997). Discourse, Videos and Talk about Sexual Violence: A Multi-disciplinary Enterprise. *South African Journal of Psychology*, 27(2), 64-74.
- Ledbetter, M. (1996). *Victims and the Postmodern Narrative, or Doing Violence to the Body: An Ethic of Reading and Writing*. New York, NY: St. Martin's Press Inc.
- Mohamed, M. S. (1976). *Nyota ya Rehema*. Nairobi, Kenya: Oxford University Press.
- Mohamed, S. A. (1977). *Asali Chungu*. Nairobi, Kenya: East African Educational Publishers.
- Mtobwa, B. R. (1990). *Dar es Salaam Usiku*. Dar es Salaam, Tanzania: Heko Publishers.
- Mosha, E. (2013). Textual Construction of Domestic Violence: Examples from Kiswahili Novels. *Katika Kiswahili*, TATAKI, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kur.45 -60
- Munganyizi, P.S. (2010) 'Rape Against Women in Tanzania. Studies of Social Reactions and Barriers to Disclosure'. PhD. Dissertaion, Uppsala University.
- Muganyizi, P. S., Kilewo, C., & Moshiro, C. (2004). Rape Against Women: The Magnitude, Perpetrators and Patterns of Disclosure of Events in Dar es Salaam, Tanzania. *African Journal of Reproductive Health*, 8(3), 137-146.
- Mugweni, E., Omar, M. & Pearson, S. (2014) Understanding Barriers to Safer Sex Practice in Zimbabwean Marriages: Implications for future HIV Prevention Interventions. *Health Education Research* 30(3) 1 -12.
- Plummer, M. L., Wight, D., Wamoyi, J., Nyalali, Ross, D. A. (2007). Are Schools a Good Setting for Adolescent Sexual Health Promotion in Rural Africa? A Qualitative Assessment from Tanzania. *Health Education Research*, 22(4), 483-499.
- Potts, A. (2001). The Man with two Brains: Hegemonic Masculine Subjectivity and the Discursive Construction of the Unreasonable Penis-self. *Journal of Gender Studies*, 10(2), 145-156.
- Reinholtz, R. K., Muehlenhard, C. L., Phelps, J. L. & Satterfield, A. T. (1995). Sexual Discourses and Sexual Intercourse: How the Way we Communicate

- Affects the Way we Think about Sexual Coercion. In P. J. Kalbfleisch & M. J. Cody (Eds.), *Gender, Power, and Communication in Human Relationship* (uk. 141-162). Hillsdale, NJ: Erlbaum.
- Ruhumbika, G. (2001). *Janga Sugu la Wazawa*. Dar es Salaam, Tanzania: Business Printers.
- Scully, D., & Marolla, J. (1993). "Riding the Bull at Gilley's": Convicted Rapists Describe the Rewards of rape. In P. B. Bart & E. G. Moran (Eds.), *Violence against Women: The Bloody footprints* (kur. 26-46). London, England: Sage.
- Walby, S., Hay, A.& Soothill, K. (1983). The Social Construction of Rape. *Theory, Culture & Society*, 2(1), 86–98.
- Weedon, C. (1997). *Feminist Practice and Poststructuralist Theory*. Oxford, England: Basil Blackwell.
- Wubs, A. G., Aarø, L. E., Flisher, A. J., Bastien, S. ... Mathews C. (2009). Dating Violence among School Students in Tanzania and South Africa: Prevalence and Socio-demographic Variations. *Scandinavian Journal of Public Health*, 37(2), 75-86.

